# Ofisi ya Elimu Maalum
# Fomu na Kifurushi cha Maelezo ya Malalamiko

*Januari 2025*

**Mpendwa (Mzazi/Mlezi/Mlalamishi):**

Asante kwa kuwasiliana na Ofisi ya Elimu Maalum (BSE, Bureau of Special Education) na kutupa fursa ya kukusaidia katika suala hili. Tafadhali kagua nyenzo zilizoambatishwa kwa umakini. Iwapo una maswali, tafadhali wasiliana na ConsultLine kupitia 1-800-879-2301 au BSE kupitia (717) 783-6913.

Mchakato wa kulalamika huanza wakati BSE inapokea fomu ya malalamiko iliyojazwa na kutiwa saini. Lazima BSE ikamilishe uchunguzi na itoe Ripoti ya Uchunguzi wa Malalamiko (CIR, Complaint Investigation Report ), ndani ya siku 60. Iwapo tutabaini ukiukaji wa masharti ya jimbo au serikali kuu, Taasisi ya Elimu ya Eneo (LEA, Local Educational Agency), yaani, Kitengo cha Kati, Wilaya ya Shule, Shule ya Chata, Ofisi ya Eneo (Philadelphia), APS, nk. zitaelekezwa kurekebisha ukiukaji huo.

Kila fomu ya malalamiko hukabidhiwa Mshauri wa Elimu Maalum aliyeajiriwa na BSE.

- Mshauri huyo atawasiliana nawe kupitia simu ili kufafanua masuala ya malalamiko. Unaweza kukutana na Mshauri ana kwa ana katika eneo la umma katika saa za kawaida za kazi.
- Mshauri atakuomba utaje jina au majina ya wengine ambao huenda wanafahamu ukweli kuhusu malalamiko na atahoji idadi fulani kati yao kabla ya kutoa ripoti. (Si lazima)
- Utatumiwa Barua ya Kuthibitisha inayotaja masuala ya malalamiko.
- Iwapo masuala yaliyowasilishwa hayawezi kushughulikiwa na BSE, utapokea barua itakayokufahamisha hivyo. Utapewa maelezo ya mawasiliano ya taasisi nyingine zinazoweza kukusaidia.
- Mshauri anaweza kufanya uchunguzi katika kituo cha LEA ili kukagua rekodi zinazofaa na kuwahoji wafanyakazi.
- Unaweza kutoa maelezo ya ziada kupitia mazungumzo au kwa kuandika kabla ya CIR ya mwisho.
- Kisha Mshauri atachanganua uhalisi na kubuni CIR iliyoandikwa.
- Mshauri atatuma CIR kwa Mkuu wa Kitengo kwa ajili ya ukaguzi na usahihishaji.
- CIR itatolewa baada ya kuidhinishwa na Mkuu wa Kitengo.

**Kusuluhisha au Kuondoa Malalamiko:**
Wahusika wanaweza kusuluhisha malalamiko wenyewe. Iwapo wahusika watasuluhisha masuala, LEA itawasilisha uthibitisho ulioandikwa ulio na saini ya mlalamishi. BSE itatoa Barua ya Suluhisho kwa mlalamishi na kwa LEA ili kufunga malalamiko.

Mlalamishi anaweza pia kuchagua kuondoa malalamiko. Mshauri atawasiliana na mlalamishi na kuomba arifa rasmi kupitia barua na BSE itatoa uthibitisho kwa mlalamishi kupitia Barua ya Kuondoa malalamiko.

**Kuongeza Muda wa Malalamiko:**
Wahusika wanaweza kuingia katika mchakato wa upatanishi wakati wowote. Wahusika wakishiriki katika mchakato wa upatanishi, au mbinu nyingine mbadala za kusuluhisha mzozo (yaani, uwezeshaji wa IEP) muda wa uchunguzi wa malalamiko unaweza kuongezwa upite siku 60 baada ya kupokea ripoti ya makubaliano kutoka pande zote mbili.

**Msingi wa Kanuni:**
Maelezo ya Malalamiko – Kwa mujibu wa Kanuni ya Serikali Kuu (34 CFR §300.153), kuna vipengee vinavyotakiwa ili kuwasilisha malalamiko. Ifuatayo ni kanuni hiyo.

**§300.153 Kuwasilisha malalamiko.**

(a) Shirika au mtu anaweza kuwasilisha malalamiko yaliyoandikwa chini ya taratibu zilizofafanuliwa katika kipengele cha §§300.151 hadi 300.152.

(b) Lazima malalamiko yajumuishe-
  - (1) Taarifa kwamba taasisi ya umma imekiuka masharti ya Sehemu ya B ya Sheria au ya sehemu hii;
  - (2) Uhalisi wa taarifa hiyo;
  - (3) Saini na maelezo ya mawasiliano ya mlalamishi; na
  - (4) Ikiwa unadai ukiukaji kutokana na mtoto mahususi-
    - (i) Jina na anwani ya makazi ya mtoto;
    - (ii) Jina la shule ambako mtoto anahudhuria;
    - (iii) Ikiwa mtoto au kijana hana makao (kulingana na maana ya sehemu ya 725(2) ya Sheria ya Usaidizi kwa Wasio na Makao ya McKinney-Vento (42 U.S.C. 11434 a (2)), maelezo ya mawasiliano yanayopatikana ya mtoto, na jina la shule ambako mtoto anahudhuria;
    - (iv) Ufafanuzi wa hali ya tatizo la mtoto, ikiwemo uhalisi unaohusiana na tatizo; na
    - (v) Suluhisho linalopendekezwa la tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kupatikana kwa mhusika wakati malalamiko yanawasilishwa.

(c) Lazima malalamiko yadai ukiukaji uliofanyika kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja kabla ya tarehe ya kupokelewa kwa fomu ya malalamiko kwa mujibu wa § 300.151.

(d) Lazima mhusika anayewasilisha malalamiko atume nakala ya malalamiko hayo kwa LEA au taasisi ya umma inayomhudumia mtoto wakati ambapo mhusika anawasilisha malalamiko kwa SEA.

**Uwasilishaji wa Washirika Wengine – Ilani ya Masharti ya Usiri:**
Iwapo mtu mwingine mbali na mzazi au mlezi atawasilisha malalamiko, mlalamishi atapokea barua kutoka kwa Mshauri wa Elimu Maalum inayotaja kuwa bila ruhusa ya mzazi ya kutoa maelezo ya siri, BSE haiwezi kumjibu moja kwa moja kuhusu malalamiko hayo.

Hata hivyo, BSE itafanya uchunguzi, itaandaa CIR ya matokeo na kutoa ripoti ya matokeo moja kwa moja kwa mzazi na kwa LEA.

**Utaratibu wa Kanuni za Serikali Kuu (CFR, Code of Federal Regulations), Mada ya 34, Sehemu ya 300 unataka:**

1. Lazima mlalamishi atie saini malalamiko kabla BSE ichunguze madai hayo.
2. Mlalamishi anatakiwa kisheria kutuma nakala ya fomu ya malalamiko kwa LEA.
3. Lazima mlalamishi apendekeze suluhisho la tatizo iwapo linafahamika na kupatikana kwa mhusika wakati malalamiko yanawasilishwa.
4. Taasisi ya umma ina fursa ya kujibu kwa kutoa pendekezo la kusuluhisha malalamiko hayo.
5. Fursa hupewa mzazi aliyewasilisha malalamiko na taasisi ya umma ili kushirika katika mchakato wa upatanishi kwa hiari.
6. Mlalamishi atapokea nakala ya Ilani ya Taratibu za Ulinzi (Procedural Safeguards Notice) kutoka ELA wakati mlalamishi anawasilisha malalamiko mara ya kwanza katika mwaka wa shule.

# Fomu ya Malalamiko

Uko huru kutoa nakala za fomu hii, kutumia karatasi za ziada au kupigia simu ConsultLine kupitia 1-800-879-2301 au Ofisi ya Elimu Maalum (BSE) kupitia 717-783-6913 ili upate nakala za ziada.

**Mbinu ninayopendelea ya kuwasiliana na Mshauri aliyekabidhiwa malalamiko haya itakuwa (Si lazima):**

☐ **Kwa simu (tafadhali weka namba):**
**Muda bora wa kupiga simu katika saa za kawaida za kazi:**

☐ **Kupitia barua pepe (tafadhali weka anwani ya barua pepe):**

☐ **Ana kwa ana kwenye kituo cha umma katika saa za kawaida za kazi.** Huenda eneo likawa jengo la shule au Kitengo cha Kati (Intermediate Unit) ili urudufishaji wa hati.

**Je, unawasilisha malalamiko haya kwa niaba ya mtoto mahususi?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana

## Tafadhali weka maelezo yako ya mawasiliano, uhusiano na mtoto, na saini yako.

**Jina:**

**Anwani:**

**Namba ya Simu:**

**Nyumbani:**

**Kazini:**

**Simu ya mkononi:**

**Barua pepe:**

**Uhusiano na mtoto au watoto:**
☐ Mzazi ☐ Wakili ☐ Mtetezi ☐ Mwingine

**Jina na anwani ya makazi ya mtoto, shule na wilaya ya shule.**

**Jina la Mtoto:**

**Tarehe ya Kuzaliwa:**

**Anwani:**

**Je, mtoto yuko shuleni sasa?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana

**Ikiwa yuko, mpango wa sasa wa mtoto uko**

**wapi: Jengo la Shule:**

**Wilaya ya Shule:**

**Shule ya Chata:**

**Je, mtoto amewekwa kwenye mpango wa elimu na Hakimu au Taasisi ya Maslahi ya Watoto?**

☐ Ndiyo ☐ Hapana

**Ikiwa yuko, mpango wa sasa wa mtoto uko wapi:**

**Mwasiliani:**

**Namba ya Simu:**

**Jaza *tu* ikiwa malalamiko yamewasilishwa kwa niaba ya mwanafunzi**

**anayebadilisha shule mara kwa mara. Mwasiliani:**

**Namba ya Simu:**

**Je, ukiukaji ulifanyika mwaka uliopita? Iwapo ni hivyo, ilikuwa tarehe ipi au karibu**

**na tarehe ipi?**

**Tarehe:**

**Ili kufafanua madai yangu, ningependa Mshauri ahoji mtu au watu wafuatao: (Si lazima)**

| Jina | Kazi/Cheo | Namba ya Simu/Anwani ya Barua Pepe |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

**Tafadhali toa taarifa kuhusu ukiukaji au tatizo, ambalo unaamini limetokea. Tafadhali weka maelezo kuhusu hali ya tatizo.**

**Tafadhali orodhesha hoja ambazo zinathibitisha taarifa yako.**

**Kadiri ujuavyo, tafadhali pendekeza suluhisho la tatizo hili iwapo linafahamika na kupatikana.**

**Lazima malalamiko haya yatiwe saini ili BSE ichunguze. Ni lazima pia utume nakala ya malalamiko haya kwa Taasisi ya Elimu ya Eneo (LEA). Kwa kutia saini hapa chini, unaashiria kwa BSE kuwa umetuma nakala ya malalamiko kwa LEA.**

______________________________________________________________

**Tarehe ya Saini**

**Tafadhali rejesha fomu kwa:**
**PDE/BSE**
**Kitengo cha Kupanga na Kufuatilia Utiifu - East**
**607 South Drive, 3rd Floor**
**Harrisburg, PA 17120**

**Barua pepe: [ra-pdespecialed@pa.gov](mailto:ra-pdespecialed@pa.gov)**

**ConsultLine – CRP**

______________________

**Vifupisho Tarehe**